MADA NA. 10 – Wajibu wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (PETS) katika kukuza Utawala Bora na Uwajibikaji

10.1 ***Wasilisho la Mada kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)*** **–Bi. Usu Mallya**
Sisi sote tunajishughulisha na PETS kwa kiwango fulani.

- ***Rasilimali*** – zilizopo mahali, ni nani anazimiliki
- ***Bajeti*** – pale tulipo kuna makundi gani, bila ya kuvaa jicho la jinsia ni vigumu kutengeneza bajeti inayokidhi, kwani jamii haiko sawa. Kuna wenye uwezo, walemavu, watoto, n.k. Je, bajeti imeshirikisha makundi haya na ni kwa kiwango gani viongozi wamehakikisha bajeti imebeba mahitaji
- ***Mchakato wa Ufuatiliaji wa Matumizi ya Fedha za Umma (PETS)*** – katika ngazi za kitaifa na halmashauri. Je, katika utayarishaji wa bajeti ni nani mshiriki mkuu? Je, masuala yanayojitokeza ngazi hii ni nani anasimamia ili kuhakikisha vipaumbele vya wananchi vinazingatiwa? Je, kilichomo kwenye bajeti kinahusu makundi gani? Kila mwanajamii ashiriki katika mchakato wa kupitisha bajeti. Viongozi, madiwani wahakikishe kwamba bajeti inabeba masuala ya wanajamii.
- ***Utekelezaji wa bajeti*** – huu ni mfumo mzima wa bajeti na takwimu, kuna mikakati gani ya ushiriki wa makundi?
- ***Hatua ya Ukaguzi*** – Je, tunafanya nini baada ya ripoti ya CAG? Tunatumiaje taarifa kuwawajibisha, kujenga mifumo ya ushiriki wa wananchi katika kufuatilia rasilimali
- ***Changamoto:*** Ni kodi zipi zinawaangukia zaidi makundi gani na pia masuala ya misamaha ya kodi.
  Ufuatiliaji wa rasilimali katika ngazi zote ni jukumu letu sisi AZAKi na ndio njia kuu ya kuleta maendeleo na kupunguza ufujaji.

10.2 Mchango kutoka TACOSODE **– Bi. Theofrida Kapinga**
PETS ni ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma. PETS inafuatilia mtiririko wa fedha kutoka Serikali kuu hadi idara hadi mtoa huduma na hatimaye mpokea huduma (kama ni shule ni hadi walimu na wanafunzi; hospitali ni wauguzi na wagonjwa). Tunataka kuona mtiririko unafikisha fedha kwa kiwango kile kile au iwapo kuna ufujaji. Lakini pia tutaangalia ubora wa huduma, k.m. tofali za inchi 5 au 6 zimetumika, au tumeezekea bati za 30G au 28G.
Matatizo ya zoezi la PETS:

- Kwa baadhi ya watendaji wa halmashauri walilichukulia zoezi hili kama halitofautiani na ukaguzi unaofanywa na CAG au TAKUKURU.
- Watendaji wengine walikuwa na wasiwasi na matumizi ya taarifa hizi, kutokana na wasiwasi huu walipenda kuomba kibali cha Kikao kizima cha madiwani. Madiwani waliunga mkono zoezi hili.
- Utunzaji wa kumbukumbu ulikuwa dhaifu na taarifa zilitofautiana. Mhazini anaweza kuwa na data tofauti na idara husika.

Zoezi la PETS haliangalii tu takwimu, bali pia je, waliopokea huduma wameridhika na vipaumbele vyao. Baada ya kufanya zoezi hili tunahitaji pia kupata mrejesho kutoka kwa jamii ili wachangie hali walivyoiona na mapungufu yaliyojitokeza.

Baadhi ya faida za PETS ni:

- PETS inakuza sauti ya watoaji na wapokeaji wa huduma
- " inakuza mifumo mizuri ya uwajibikaji, ufanisi kuongezeka
- " inaongeza ushiriki na mawazo ya wananchi
- " ni huduma inayotokana na uhitaji (demand-driven)

Baadhi ya mapungufu ya PETS:

- PETS haielekezi jinsi ya kuwawajibisha wanaofuja mali ya umma
- Pamoja kwamba PETS inaimarisha mifumo ya kijamii na ni muhimu kwa jamii lakini tusitegemee fedha za wafadhili. Halmashauri ziwe na mfumo wa kuhakikisha PETS inafanyika kwa kutumia rasilimali zao.

***10.3 Uzoefu kutoka FOGOTA* – Bw. Emmanuel Kazungu**

Haki na uhalali wa kufuatilia matumizi ya fedha za umma iko katika Katiba, ibara ya 18; Sheria ya Fedha za Umma, 2001 na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na. 9 ya 1982 na Memoranda ya Serikali za Mitaa, 1997. FOGOTA imejihusisha kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya PETS katika Halmashauri za Wilaya sita: Bukoba Mjini, Bukoba Vijijini, Muleba, Tandahimba, Nanyumbu na Ruangwa. Sekta mbili zilifanyiwa ufuatiliaji – VVU/UKIMWI na Elimu.

Changamoto za PETS:

- Ugumu wa upatikanaji wa taarifa za mapato na matumizi za Halmashauri kutoka kwa watendaji. Hii inatokana na mfumo mgumu wa utoaji taarifa za fedha
- Lugha inayotumika ya Kiingereza haieleweki kwa wananchi wa kawaida hata madiwani
- Watendaji kutokuwa na imani na wafuatiliaji wakidhani ni wakaguzi wa hesabu na kuwa tishio kwa maslahi yao.
- Uwezo mdogo wa watendaji wa kuhifadhi kumbukumbu muhimu – ngazi ya kata, kijiji, zahanati na shule.
- Ufuatiliaji wa ripoti za PETS – baada ya mrejesho wa taarifa ya PETS, nini kinafuatia? Taarifa inapelekwa wapi? Lazima tufike mahali ambapo wafujaji wa rasilimali za umma wanapelekwa mahakamani.
- Uendelevu wa PETS – wananchi wanatakiwa hatimaye waweze kusimamia wenyewe mchakato mzima wa PETS.

***10.4 Maoni kutoka Policy Forum* – Bw. Marcossy Albany**

- PETS ni hatua za wananchi katika vikundi vyao (AZISE, AZAKi, CBO, FBO, n.k.) kufuatilia matumizi ya rasilimali zao
- Mpango huu ni haki na wajibu wetu kama wananchi – umeanishwa katika sera, sheria na taratibu za nchi.
- Ushiriki wa wananchi pia ni pamoja na PETS.
- Mwananchi ndio mhimili mkuu wa usimamizi wa fedha na rasilimali za umma.

Changamoto:

- Yapo mapungufu katika maeneo mbalimbali ya kiutendaji, k.m. Shilingi bilioni 2.9 hazikuonekana katika fedha za matumizi mkoani Kagera! na pia matumizi ya hovyo.
- Mapungufu ya kiutaratibu
- Taarifa zinazotolewa kutoeleweka
- Ucheleweshaji wa utoaji wa rasilimali – k.m. halmashauri inapokea fedha robo tatu ya bajeti kukiwa kumebaki siku 33 kufikia mwisho wa mwaka wa fedha.
- Maagizo na amri mbalimbali zinazowachanganya watendaji kutoka serikali kuu, TAMISEMI n.k.
- Uwezo mdogo wa AZAKi kufanya ufuatiliaji hasa asasi za ngazi za msingi.
- Matumizi mabaya ya taarifa hizi – kimsingi taarifa hizi zinaelekeza marekebisho ya kiutendaji na hazina maudhui ya kisiasa.
- Je, tuliowachagua kama viongozi wetu wana uwezo wa kusimamia shughuli zetu?

Tufanye nini?

- Serikali itambue kwa vitendo mchango wa Asasi za Kiraia katika Maendeleo ya Jamii. Vitendo hivyo ni pamoja na kutoa bajeti kwa AZAKi zinazofuatilia PETS
- AZAKi zijizatiti bila hofu wala kuchoka kufuatilia PETS, na tunapotishwa maana yake tunatimiza wajibu wetu.
- Hatua tatu za ufuatiliaji wa uwajibikaji kijamii (social accountability monitoring) ziheshimiwe – ambazo ni upangaji, matumizi na mapato, na ufanisi.

10.5 Mjadala wa Pamoja, Maoni na Mapendekezo

- Huwezi kufanya maamuzi yaliyo sahihi au ya kuwawajibisha watendaji bila ya sheria. Ili tuimarishe uwazi wa taarifa tunahitaji kupata sheria ya habari. Pia hakuna sheria inayozungumzia unyeti wa taarifa na taarifa zinatakiwa kutolewa katika ukomo wa kipindi gani?
- Je, sisi AZAKi tumeshirikiana vipi na wawakilishi, madiwani, ili watambue mapungufu haya ya PETS.
- Dhana ya PETS tuipanue zaidi. Rasilimali tunazofuatilia isiwe fedha tu, bali ijumuishe rasilimali watu, vifaa n.k. Tumefuatilia kwa kiasi gani misitu, wanyama pori (pembe na ngozi), samaki, n.k.
- Kuna changamoto zaidi kwa wafuatiliaji wa PETS baada ya kuanzishwa kwa mfuko wa jimbo – je, tumejipanga vipi?
- Katika miradi mikubwa k.m. TASAF, tuwe na uwezo wa kufuatilia ili tuone ubora wa huduma
- AZAKi zinazojishughulisha na PETS zijengewe uwezo wa kufanya utetezi na ushawishi
- Kuna umuhimu wa kuangalia rasilimali kwa upana zaidi, kujenga nguvu ya pamoja katika sekta kama za madini, misitu ili kuweza kupambana na nguvu kubwa. Kutumia mashirika ya kimataifa na vyuo vyetu kufanya utafiti. Vyombo vya habari pia ni muhimu katika kusaidia ufuatiliaji wa PETS na kudai kuwajibishwa kwa wafujaji.

- Vikao vya madiwani vihusishwe katika PETS. Serikali za vijiji ziwezeshwe kufuatilia.
- PETS imejikita zaidi katika kufuatilia matumizi na kusahau usimamizi. Wananchi waamshwe na kushiriki kikamilifu. AZAKi nazo zishiriki katika vikao vya kijiji/kata na mitaa.
- Uwezo mdogo wa watendaji vijijini kunatokana na elimu duni. Wasomi wahamasishwe kugombea nafasi hizi za chini na sio ubunge tu.
- Rasilimali za kuhudumia makundi yenye mahitaji maalumu – tutumie PETS kubadilisha mfumo wa jinsi rasilimali zinavyokusanywa na zinavyotumika. Tushirikiane na jamii katika kuelekeza mahitaji kwa makundi tete.
- Ili tuweze kutekeleza PETS na kuwajibisha wanaofuja rasilimali za umma, sisi wenyewe tunatakiwa tujisafishe kwanza.
- Taarifa za PETS pia iwe kigezo kimojawapo cha kupata fedha/rasilimali kutoka serikalini.
- Tunapendekeza pawepo na ***Tuzo ya Halmashauri Bora*** – itatoa changamoto ya kuongeza uwajibikaji na ufanisi.